



MAJILIO 2026 – WIKI YA 1

KES HENI!

Wito wa Ulimwengu Mzima wa Uwakili Mwaminifu

Marko 13:24–37



**“Na jina lake
Mataifa watalitumainia.”**

Mathayo 12:21 (SRUV)



Leo tunawasha mshumaa wa TUMAINI.

Tumaini si jambo la kukaa tu bila kufanya chochote; ni la vitendo, linahitaji kuwa macho na kutazamia kwa matarajio. Yesu anatuita, “Kesheni!” na tuendeleo kuwa macho kwa ajili ya utume wake na kurudi kwake.



**Tumaini hili si kwa ajili yetu tu. Ni kwa
ajili ya Kanisa la ulimwenguni kote:**

waumini kutoka mataifa yote wanaotumaini, wanaoomba na
wanaotumikia. Kutoka Nairobi hadi Nashville, kutoka São
Paulo hadi Seoul, sisi sote ni sehemu ya familia ya Mungu,
tukiendelea kukesha kwa uaminifu.



**Tunawasha mshumaa huu kwa
ajili ya wamisionari wanaopeleka
tumaini kuvuka mipaka,**

**kwa ajili ya makanisa yanayoanzishwa katika maeneo
yenye changamoto, na kwa ajili ya kila moyo ambao bado
unasubiri kusikia jina la Yesu.**



Mungu wa tumaini, tunakushukuru kwa kumtuma Yesu, nuru katika giza letu.

Liamshie Kanisa lako kushiriki katika utume wako wa ulimwenguni kote. Tumaini letu liwe la vitendo: tukilinda ukweli, tukiwatumikia wengine na tukikesha kwa furaha. Mshumaa huu utukumbushe kwamba ahadi zako ni kwa ajili ya watu wa mataifa yote, na kwamba tumeitwa kuzishiriki.

Amina.



